

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

JAMBO AMBALO HALIBADILIKI HATA WAKATI HUU WA COVID-19

Virusi vya ugonjwa wa koronavirus—COVID-19—vilizuka jijini Wuhan, Uchina, mwezi wa Novemba, 2019. Kutoka hapo virusi hivyo vilisambaa kwa haraka sana na kuwaathiri watu wengi kote duniani. Kufikia wakati wa kuandika jalida hili kuna watu zaidi ya laki moja ambao inajulikana kwamba wameambukizwa virusi hivyo, na vimesababisha vifo vya watu makumi ya elfu. Zaidi ya hayo, kila siku tunaona kwamba kuna maelfu ya maambukizi mapya, na inatarajiwa kwamba idadi ya visa hivi vipya, na vifo vinavyosababishwa na virusi hivyo vya covid-19 vitazidi kupanda kwa haraka.

Katika jitihada za kupunguza kusambaa kwa virusi hivyo, serikali nyingi za dunia zimeamuru biashara kufungwa na pia kukataza kufanyika kwa mikutano. Pia serikali nyingi za miji zimewataka raia wake kukaa nyumbani na kutofanya safari, isipokuwa safari za dharura za kupata chakula na huduma zingine za lazima. Mambo haya yote yamefanya uchumi wa ulimwengu kuzorota na watu wengi wamepoteza kazi zao, na hata shughuli nyingine ambazo huwaletea watu chakula cha kila siku zimeathirika sana. Nayo mikutano ya kijamii ya watu kufurahi pamoja imewekewa mipaka, na hata milango ya makanisa mengi kufungwa kwa amri ya serikali. Maisha ya kawaida kama

tunavyoyajua sasa yamebadilika kwa ghafla kwa vipengele kadhaa wa kadhaa. Kwa kweli tunaishi wakati wenye maswali mengi na woga mwingi umetapakaa kila mahali.

Kusema kweli kuna mambo mengi ambayo kila siku yanabadilika maishani mwetu, lakini mabadiliko hayo magumu yanapofanyika kwa haraka hivi kote ulimwenguni, ndipo tunatambua kwamba mambo ambayo yanaweza kubadilika ni mengi mno—uhai, kifo, afya, ibada za kanisa, mahusiano ya watu, kazi, kustaafu, na hata mahitaji ya kila siku kama vile chakula na maji.

Kwa kweli mambo kubadilika ni sehemu ya maisha haya, lakini hata katika mambo haya ambayo yanavuruga maisha yetu kuna jambo moja ambalo linaendelea kwa uhakika kabisa, na ambalo kamwe halibadiliki

— Mungu mwenyewe. “Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu” (Malaki 3:6). Upendo wake na jinsi ambavyo anawatunza watu wake ni mambo ambayo hayabadiliki. Yeye ni ngome wakati wa shida, na anawapatia watu wake chakula cha kila siku wakati wa njaa. Watu wengi wameingwiwa na woga mwingi na wanajihisi kwamba hawana tumaini. Lakini wewe mtoto wa Mungu, hata ingawa unaishi katika siku hizi ambazo hazina uhakika wa maisha, kumbuka kwamba wewe ni msafiri na mgeni katika maisha ya sasa. Kila siku sisi tunaweza kumtegemea Yeye ambaye habadiliki, Yeye ambaye atahakikisha kwamba tumepita siku hizi ngumu kwa amani na ushindi wa kiroho.

Kama jinsi mwandishi mmoja wa nyimbo ameandika na kusema, “Mungu tayari ahasema, ‘Wewe utashinda!’” —mws



FANYA MAMBO HAYA MATANO



SAIDA KUKOMESHA KORONA VIRUS

1. **Mikono** Nawa mara nyingi.
2. **Kiwiko cha mkono** Koholea hapo.
3. **Uso** Usiguze.
4. **Nafasi** Jipe nafasi ya usalama.
5. **Nyumbani** Kaa humo inawezekana.

World Health Organization

Mifano Inayotolewa na Biblia ya Mkristo kuwa Mwananchi Mwema 2 Tahariri 3

Kuhusu Maambukizi ya COVID-19; Faraja Iletwayo na Ahadi Zake Mungu; Katika Wakati Kama Huu 4

Amka Uombre 5 Imani Yetu Iko Wapi 6

Woga Umetuzingira; Nyinyi ni Chumvi ya Ulimwengu 7

Kuwa Mbali/Kupatana Mavazi Yaliyopangwa Vizuri 8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

MIFANO INAYOTOLEWA NA BIBLIA YA MKRISTO KUWA MWANANCHI MWEMA

Serikali za nchi nyingi zimesema kwamba kusiwe na makusanyiko ya watu wakati huu wa vurugu iliyoletwa na virusi vya korona. Lakini kumekuwa na mjadala wa hivi karibuni: je, sisi kama Wakristo tunastahili kufuata maagizo hayo na kuahirisha ibada zetu za kawaida, au tunahitaji kukaidi amri hizi za wanadamu ili tumwabudu Mungu makanisani mwetu? Sisi kama mwili wa Kristo tutakuwa tukitoa mfano na ujumbe gani kwa ulimwengu na majirani zetu ikiwa tutakutana kwa ajili ya ibada huku tukikaidi serikali zetu za kidunia? Je, jambo hilo litaonyesha jinsi ambavyo tumejitolea kwa Mungu au litakuwa dhahirisho la jinsi tulivyo na roho kaidi zenye kuasi?

Kwa upande mmoja mtume Petro alikatazwa na viongozi wa kiserikali kuhubiri injili. Lakini yeye akajibu, “Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu” (Matendo 5:29). Nayo Waebrania 10:24 inasema kwamba, “Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine.” Lakini kwa upande ule mwingine Yesu alifundisha kwamba tunahitaji kunyenyekea chini ya mamlaka ya wanaotusimamia. Naye mtume Paulo akizungumza kuhusu serikali alisema maneno yafuatayo katika Warumi 13:1, “Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo umeamriwa na Mungu.”

Ni dhahiri kwamba Maandiko yanafundisha kwamba Wakristo wawe wananchi wazuri, na pia kwamba wanahitaji kufuata sharia na amri za kweli za serikali zao. Jambo hili halitegemei ikiwa tunakubaliana au kutokubaliana na matakwa hayo ya kiserikali. Lakini ikiwa serikali itakataza watu kuhubiri injili kwa kusudi la kukatisha ujumbe wa Kristo (kama ambavyo serikali ya wakati wa Mtume Petro ilijaribu kufanya), Wakristo wanastahili kupuuzwa amri hiyo kwa moyo mkunjufu. Lakini mambo haya ya covid19 hayalingani na hivyo, na pia kusudi la amri za serikali kuhusiana na kufunga makanisa kwa muda mfupi hayaambatani na kusudi la kupinga ujumbe wa Kristo. Kusema kweli kufunga makanisa ni jambo la mtu kumpenda jirani yake kwa kiwango kikubwa hivi kwamba yeye hataki kusambaza virusi hivyo kwa jirani huyo.

Wakristo wana jukumu la kunyenyekea chini ya mamlaka (ya mpito) ya wanadamu katika kukabiliiana na janga hili lililotupata na kutumia njia mbadala za kufanya ibada za kanisa kwa njia za kidijitali ambazo zitawawezesha kushiriki kama ndugu na dada katika Bwana. Mtume Petro alitoa muhstasari kwa jambo hili katika 1 Petro 2:13-17 “Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana; ikiwa ni mfalme, kama mwenye cheo kikubwa; ikiwa ni wakubwa, . . . Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu; kama walio huru, ila wasioutumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya, bali kama watumwa wa Mungu. Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme.” –mws

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the-gospeltruth.org

Tahariri (Toleo Maalum)



Ni nani atakayetenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? . . . Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza

kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu. -Warumi 8:35-39

Ni faraja na hakikisho kubwa kiasi gani kujua kwamba hakuna jambo ambalo linaweza kututenganisha na upendo wa Mungu. Ingawa tutapatana na mambo magumu maishani mwetu, lakini hakuna nguvu, virusi, kupoteza kazi, na mambo mengine kama hayo ambayo yataweza kuiba wokovu wa mtoto wa Mungu. Kuna nguzo la tumaini ambalo linapatikana ndani yake Kristo, na mbele yetu kuna siku (za milele) ambazo zitamejaa utukufu ikiwa tutadumu huku tutikiwa waaminifu kwa Bwana wetu na Kiongozi wetu.

Katika robo hii ya mwaka Bwana aliniongoza kuchapisha toleo maalum la Ukweli wa Injili ambalo litakuwa na mpangilie tofauti na hata kushughulikia mambo tofauti na matoleo yale mengine. Ulimwengu wetu umepatwa na hali mbaya na ya hatari kutokana na kusambaa kwa ugonjwa wa virusi vya koronavirus (COVID-19), na watakatifu wa Mungu kwa sasa wanaishi katika siku ambazo hazina uhakika na udhabiti. Ingawa kwa kweli hatuna majibu ya maswali yote kuhusiana na sababu na kusudi za matukio tunayopata maishani, sisi tunajua kwamba Mungu atafanya kazi kwa ajili ya manufaa ya roho za wanadamu. Toleo hili lina makala ya waandishi tofauti tofauti ambao ni wahudumu wa Kanisa la Mungu kutoka sehemu tofauti ulimwenguni. Makala yenyewe yameandikwa ili kuwatia moyo, kuwahimiza, na hata kuwafariji watakatifu wa Mungu katikati mwa mateso ambayo yameletwa na virusi vya koronavirus, COVID-19. Ni tumaini langu kwamba toleo hili litakuwa la baraka maalum na litawahimiza watoto wa Mungu kwa njia maalum.

Hata ingawa baadhi ya watu wamepatwa na wasiwasi mwingi na masumbufu mengi mimi ninakuhimiza uweke tumaini lako kwa Bwana Yesu, na uishi kwa utulivu bila wasiwasi huku ukiendelea kuishi ndani yake. Katika siku hizi zenye masumbufu, ikiwa ni katika uhai au mauti, kuna ujuzi ambao mtu anaweza kuwa nao wa kuwa na amani isiyoeleweka kwa akili za kibinadamu. Na kama hujaokoka kutoka dhambini huu ndio wakati mwafaka wa kutubu na kukubali kipawa cha wokovu. Kama ungali unasumbuka na kuogopa hebu jua kwamba Mungu anakujali sana. Yeye alitupatia Roho Mtakatifu awe mfariji wetu wa kutuwezesha kutuliza roho zetu za kibinadamu hata wakati mtu anapambana na mawimbi maishani.

Ulimwengu huu ushawahi kupambana na hali ngumu nyingi na hata majanga mengi. Sisi hatutaki kuwa chanzo cha kuwaletea watu woga, lakini pia hatutaki kuwa watu ambao hawatilii maanani uzito na matatizo ambayo yanaletwa na virusi hivi. Ni ombi letu kwamba Bwana atabadilisha janga hili ili na kuwaletea watu wake furaha, na pia kufanya watu kuamka na kutambua mahitaji yao ya kiroho yaliyomo katika nafsi zao.

Hebu basi tuendeleo kuombeana na kumkaribia Bwana wetu. Mungu anatutegema sisi sote ili tuwe nguzo muhimu za kanisa na ambazo zinaweza kutegemewa. Tunahitaji kuwa wanajeshi shupavu wa msalaba, ambao kamwe hawatingisiki hata katika wakati huu wa shida. Mungu na awabariki enyi ndugu na dada zangu.

Michael W. Smith

Aprili 2020.



“WAANGALIENI NDEGE WA ANGANI, YA KWAMBA
HAWAPANDI, WALA HAWAVUNI, WALA HAWAKUSANYI GHALA-
NI; NA BABA YENU WA MBINGUNI HUWALISHA HAO. NINYI JE! SI
BORA KUPITA HAO?” MATHAYO 6:26



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujiandikisha na

kupata jarida

za mbele.

FARAJA ILETWAYO NA AHADI ZAKE MUNGU

NDUGU VALERI GLAAS (UJERUMANI)



Ingawa ulimwengu wote umeshikwa na masumbufu, wasiwasi, maafa, na mambo mengine kama hayo ambayo yatazidi kutuzingira hadi hapo jambo hili litakapofikia kikomo chake, Mungu ndiye nguvu za watu wake, na Yeye ndiye nguvu za wale ambao wana moyo safi.

“Mwili wangu na moyo wangu hupunguka, bali Mungu ni mwamba wa moyo wangu, na sehemu yangu milele . . . nami kumkaribia Mungu ni kwema kwangu; nimefanya kimbilio kwa Bwana MUNGU, niyahubiri matendo yako yote” (Zaburi 73:26,28).

Kuna ahadi nyingi zinazopatikana katika Zaburi 91 na ambazo zinaweza kutumika katika shida ambazo zimetupata sasa. Amebarikiwa yule mtu ambaye anaweza kuweka tumaini lake kwa Bwana na kuitisha ahadi zake. Mungu mwenye nguvu zote ameahidi kwamba Yeye ndiye makazi na ngao yetu wakati wa mahitaji, wakati wa magonjwa na tauni; na sisi tutakuwa salama ikiwa tutazidi kutegemea ahadi zake.

“Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.” (2 Wakorintho 1:20).

Je, si ni jambo lenye utukufu mkuu ikiwa sisi tutaendelea kudumisha amani ya Mungu mioyoni mwetu katika nyakati hizi za shida, na ikiwa mioyo yetu itazidi kujaa nyimbo za ukombozi wake?

“Ndiwe sitara yangu, utanihifadhi na mateso, utanizungusha nyimbo za wokovu” (Zaburi 32:7). Bwana atabariki kila mmoja ambaye tumaini lake ni kwake. Tunaomba Mungu atujaze ujasiri na ushupavu wa kumwabudu Bwana na kumsifa hata katika nyakati tunazoishi.

“Walakini nitamfurahia BWANA nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu” (Habakuki 3:18).

KUHUSU MAAMBUKIZI YA COVID-19

NDUGU CHINWENDU NWACHUKWU (NIGERIA)



Ni jambo la kushangaza kwamba ulimwengu wetu umekumbwa na ugonjwa mwingine wenye madhara ya kuua na ambao ikiwa Bwana hatatuonyesha rehema zake watu wengi watakuwa.

Sisi kama watoto wa Mungu tuna mwito wa kufanya sala kwa Mungu kwa ajili ya siku hizi ambazo tunaishi ndani mwake. Ingawa kuna dhana tofauti kuhusiana na chanzo na lengo la ugonjwa huu -- kama ugonjwa huu ni wa kiasili au uliundwa na wanadamu, kunalo jambo moja ambalo ni la hakika kabisa, Bwana mwenyewe ameruhusu ugonjwa huu kutokea katikati mwetu. Wiki kadhaa kabla ya ugonjwa huu kusambaa sana mawazo yangu yaliongozwa kutafakari kuhusu andiko linalopatikana katika Ezekieli 14:12-20.

“Neno la BWANA likanijia, kusema, mwanadamu, nchi itakapofanya dhambi na kuniasi, kwa kukosa, nikaunyosha mkono wangu juu yake, . . . au nikipeleka tauni katika nchi ile, na kumwaga ghadhabu yangu juu yake, kwa damu; ili kuwakatilia mbali nayo wanadamu na wanyama; wajapokuwamo ndani yake Nuhu, na Danieli, na Ayubu, kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, hawatakoa wana wala binti; watajiokoa nafsi zao tu kwa haki yao.”

Janga hili linastahili kufanya mioyo yetu kuwa na mizigo mizito ya kumtafuta Bwana ili atuonyeshe rehema zake. Kulingana na jinsi maradhi haya yamesambaa, na ukweli kwamba wanadamu kwa sasa hawana uwezo wa kukatisha maambukizi haya, jambo hili ni dhihirisho kwamba wanadamu ni viumbe dhaifu, viumbe visivyo na uwezo, ukweli ambao si rahisi mwanadamu kukubali.

KATIKA WAKATI KAMA HUU

NDUGU BARTH NWACHUKWU (NIGERIA)



“Nitayainua macho yangu niitazame milima, msaada wangu utatoka wapi? Msaada wangu u katika BWANA, aliyezifanya mbingu na nchi. Asiuache mguu wako usogezwe; asisinzie akulindaye” (Zaburi 121:1-3).

Wana wa Israeli walivamiwa na nyoka wakiwa huko jangwani na wakamlilia Mungu ili awape msaada, “Bwana akamwambia Musa, jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi” (Hesabu 21:8). Bwana wetu Yesu Kristo pia alitumia mfano huo kutufaraji na kusema,

“Vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye” (Yohana 3:14-15).

Hebu tuwe na uhakika kwamba tuna Baba ambaye anapenda watoto wake katika hali zozote zile walizomo. Katika nyakati kama hizi tunazoishi hebu basi waume wote kila mahali “wainue mikono iliyotakata” kwake Mungu ambaye ndiye hujibu maombi.

AMKA UOMBE



NDUGU PETER AKWEYONA (KENYA)

Kote nchini Kenya watu wanaishi kwa woga, kwa kutojua kile ambacho kitawapata siku inayofuata. Kila siku tunaona mahali tofauti kunafungwa, na hata ibada za kanisa zinafungwa katika jitihada za kuzuia maambukizi ya virusi vya koronavirus—COVID19. Lakini Bwana anatomia virusi hivi kuwarudisha matajiri na maskini katika mahali pa toba. Hebu basi watakatifu wote ulimwenguni wasiogope, bali wainuke na kuomba ili Shetani aweze kukemewa. Kupitia kwa damu yake Yesu sisi tumeponywa.

Hebu basi tutazame aya ya Biblia ambayo itatupatia faraja. “Kwa maana mimi, BWANA, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia, Usiogope; mimi nitakusaidia” (Isaya 41:13). Hata wakati kuna tisho la magonjwa na kifo, kuna uwezo wa kiungu wa kuleta uponyaji. Hii ndiyo sababu Kanisa la Mungu linahitaji kuchukua muda

kufunga na kuomba kwa ajili ya watakatifu wote ulimwenguni. Mungu tayari ameandaa jibu kwa ajili ya janga hili, na Yeye yuko tayari na analo shauku la kuwaokoa wanadamu wake. Hii ndiyo sababu watakatifu kamwe hawastahili kuishi kwa woga.

Katika Matendo 27:22 mtume Paulo alizungumza akiwa kwenye dhoruba baharini na kusema: “Sasa nawapeni shauri, iweni na moyo mkuu, kwa maana hapana hata nafsi mmoja miongoni mwenu atakayepotea, ila merikebu tu.” Tunajua kwamba katika mataifa mengine tutawapoteza watu, lakini katika Bwana kuna uhai hata baada ya kifo. Ujumbe kwa waumini wote ni kwamba huu ni wakati wa kuamka . . . basi amka na uombe ili ugonjwa huu hatari ukome kwa jina la Yesu.

Mungu abariki ulimwengu. Na abariki watakatifu wake. Na pia abariki kazi ya injili. Kwa jina la Yesu Kristo sisi tumewaombea. Amina.

“NIKIZIFUNGA MBINGU ISIWE MVUA, TENA NIKIAMURU
NZIGE KULA NCHI, AU NIKIWAPELEKEA WATU WANGU
TAUNI; IKIWA WATU WANGU, WALIOITWA KWA JINA LANGU,
WATAJINYENYEKESHA, NA KUOMBA, NA KUNITAFUTA USO, NA
KUZIACHA NJIA ZAO MBAYA; BASI, NITASIKIA TOKA MBINGUNI,
NA KUWASAMEHE DHAMBI YAO, NA KUIPONYA NCHI YAO.”

– 2 KUMBUKUMBU LA NYAKATI 7:13-14

NDUGU SHAHZAD BABAR (PAKISTANI)



Roho Mtakatifu alinilitea andiko kutoka 2 Mambo ya Nyakati 7:14. Ni muhimu kwetu kuendelea kufunga na kuomba. Tunahitaji pia kuwa waaminifu kwa Neno lake

Mungu, hakuna haja ya kuogopa, badala yake tunahitaji kuwa waaminifu.

Tunaomba Bwana kwamba damu yake takatifu itakuwa juu ya kila mmoja wetu na kutupatia usalama. Bwana akulinde kwa jina lake Yesu. Amina. Salamu ziwafikie watakatifu wote wa Kanisa la Mungu.

NDUGU MASTER GUSTOR (MALAWI)



Nawaandikia nyinyi nyote ulimwenguni wakati huu ambapo tayari baadhi ya nchi zimepatwa na maradhi ya COVID-19. Sisi Wakristo tunahitaji kuomba kwa ari na imani kulingana na jinsi ambavyo Maandiko yanasema katika 2 Mambo ya Nyakati 7:13-14.

Kamwe tusichoke katika siku hizi za mwisho. Mungu atatufadhili. Kumbuka kwamba Daudi alishinda vita dhidi ya Goliathu wakati yeye alimtegemea Mungu. Hebu kumbuka kwamba chote ambacho mwanadamu hawezi kufanya Mungu anaweza.

Ombi langu kwa Wakristo wote ulimwenguni ni kwamba tuungane mikono na kuomba dhidi ya koronavirus. Mungu atajibu maombi yetu. Tunamwomba Mungu abariki nchi zetu.

IMANI YETU IKO WAPI

NDUGU IVAN ECK (KANSAS, MAREKANI)



Tunajua kwamba watu wengi wana maswali mengi kuhusiana na maradhi ya virusi hivi ambayo yametapakaa kila mahali ulimwenguni. Hata ingawa kuna sababu nzuri za sisi kuwa waangalifu, Mungu hataki roho zetu zigandamizwe na kuteseka kutokana na woga uliopo

mioyoni mwetu. Hii ndio sababu mimi nauliza swali hili, “Je, tunahitaji kufanya nini katika siku hizi ambazo sasa tunaishi na ambamo hatuna uhakika wa maisha?”

Biblia ina mifano mingi ya watu wa Mungu ambao walikumbana na nyakati ambazo zilikuwa na woga mwingi. Lakini hata katika siku hizo za woga watu wa Mungu walijifunza kumtumaini Mungu wa mbinguni. Tunapotazama siku zilizopita na kuona mfano wa jinsi Mungu aliwasaidia watu wake tunahitaji kuchukua muda wetu na kumtazamia Yeye ili tupate ujasiri!

Tunaona mwongozo mzuri katika sura ya 12 ya kitabu cha Waebrania. Hapo tumeagizwa kuweka kando mizigo na dhambi zetu zinazotwandama. Tunaambiwa kwamba mambo haya mawili yatatuzuia kupata ushindi wa kiroho. Baadaye tunaambiwa kwamba tunahitaji kufanya mbio ambayo imetegwa mbele zetu kwa subira, huku tukiwa na nia na kusudi la kumtazama Yesu ambaye ndiye mwanzilishi na mkamilishi wa imani yetu!

Mimi nina uhakika kwamba Bwana angetaka turuhusu shida ambazo zimetukumba kuamsha roho zetu tena ili tumtumaini Mungu kwa kiwango cha juu zaidi. Mwanazaburi aliandika na kusema “Siku ya hofu yangu nitakutumaini Wewe” (Zaburi 56:3), na tena “Uliposema, nitafuteni uso wangu, moyo wangu umekuambia, BWANA, uso wako nitautafuta” (Zaburi 27:8).

Watakatifu wa Mungu, hebu mpate hili himizo! Mimi najua kwamba Mkombozi wetu aishi! Kiongozi wa wokovu wetu

ndiye mwenye nguvu zile ambazo zilifungua njia katika Bahari ya Shamu! Yeye ndiye alifungua macho ya vipofu na kufanya viwete kurukaruka kwa furaha! Huku akiwa na ujasiri mkubwa Yeye alisimama mbele ya watu waliokufa na kuwaita wakarudi kuwa hai! Yeye pia aliwarehemu waliokuwa na makosa na waliodhihakiwa! Aliwashangaza wenye hekima kwa majibu yake rahisi! Akamkomboa mtu mwenye mapepo mengi na kumrudishia akili timamu! Yeye ndiye ngome na mnara wetu unaofika juu kabisa! Ni kiongozi wetu ambaye haoni aibu tukimwita ndugu yetu! Ni “Rafiki aambatanaye na mtu kuliko ndugu” (Mithali 18:24). Yeye alipigana na Shetani huko jangwani na kumshinda! Alienda msalabani na kutoa maisha yake kama dhabihu kwa ajili ya watu wengi! Akakumbana na kifo na kukiondolea uchungu wake! Akafika kwa wafu na kutoka tena akiwa hai! Amefufuka! Ameleta mwisho wa vita! Yeye ni Mfalme wa Amani. Yeye ni mfalme mkuu aliyebarikiwa! Ni Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana! Yeye ni Mwanzo hadi Mwisho! Yeye ni Mwokozi wangu!

Yoshua pamoja na wana wa Israeli walifika mahali pa kufanya uamuzi. Naye Yoshua akatoa uamuzi wake dhahiri, “Lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA” (Yoshua 24:15).

Enyi wapendwa wangu, hebu niulize kwa upole, “Imani yetu iko wapi?”

Bwana anafanya mwito kwetu. Ni mapenzi yake kwamba tutumie nyakati hizi kujirudia wenyewe kwa ukweli; tunahitaji kujichunguza ikiwa tuko ndani ya imani au la. Je, sisi tumesimama wima katika Mwamba Yesu Kristo?

Tunaomba kwamba utapata himizo.

Mungu abariki kila mmoja wetu!

UJUZI WA MAMBO MAGUMU

NDUGU W. S. VEDHA (BARA HINDI / INDIA)



Umri wangu ni karibu miaka 65 na nimekumbana na mambo mengi magumu katika maisha yangu ya Kikristo. Maambukizi ya ugonjwa wa koronavirus yametufundisha masomo mengi kwa muda wa miezi hii miwili. Ndiposa wengi tunafanya sala kwa Mungu huku tukiwa na swali, “Je, hizi ni siku za mwisho? Kurudi kwa Yesu kumewadia?” [“Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake” Mathayo 24:36.]

Katika huduma yetu ya kanisa na ambayo imedumu kwa muda wa miaka 45, hatujawahi kamwe kukosa kuhudhuria ibada hata moja ya Jumapili. Lakini Jumapili iliyopita sisi tulikomesha ibada ya Jumapili kutokana na amri ya serikali. Hili ni jambo ambalo liliniletea uchungu mwingi moyoni.

Enyi wenzangu watakatifu wa Mungu, ninawaomba muombee Bara Hindi (India). Sisi tunaomba kwa ajili ya hali zote zilizoko ulimwenguni kote. Mungu ndiye mwenye nguvu zote. Yeye hufanya miujiza kwa manufaa ya watoto wake. Amina.

“MAGOR-MISSABIBU” : WOGA UMETUZINGIRA

NDUGU JOHN VARGHESE (BARA HINDI / INDIA)



Yeremia 20:1-3 inasema, “Basi Pashuri, mwana wa Imeri, kuhani, aliyekuwa msimamizi mkuu katika nyumba ya BWANA . . . ndipo Pashuri akampiga Yeremia, nabii, akamtia katika mkatale . . . ndipo Yeremia akamwambia, BWANA hakukuita jina lako Pashuri, bali Magor-

misabibu.”

Ulimwengu wote umejaa woga na tisho la COVID-19. Maradhi haya yamesababisha vifo vya maelfu ya watu, na wengi zaidi wanateseka kwa sababu wamezingirwa na shida zilizotokana na ugonjwa huu. Viongozi wa kiserikali na watawala wengine wamechukua hatua za dharura ili kukatisha au kushinda maambukizi haya hatari ili kuokoa maisha ya watu.

Wakati Mungu alituma mabaa katika nchi ya Misri kwa njia ya Musa, waganga wa Mfalme Farao walijaribu kumwiga kwa kujaribu kushinda mabaa hayo, lakini kamwe hawakufaulu. Mwishowe ikawabidi kusema, “Jambo hili ni chanda cha Mungu” (Kutoka 8:19). Nao wakati wa Nuhu Mungu alitazama maovu ya mwanadamu yalivyozidi duniani, akaamua kuangamiza ulimwengu kwa

njia ya mafuriko (Mwanzo 6:5-6). Vile vile Mungu aliamua kuangamiza Sodoma kwa njia ya moto baada ya kuona uovu wa watu wa mji huo. Kulingana na nabii Ezekieli zaidi ya dhambi za ushoga watu wa Sodoma walifanya dhambi za kuwa na kiburi, pupa, kustarehe wakati mwingi, na kutofanya kazi, na kufikia hata kuwagandamiza wenzao (Ezekieli 16:49). Yesu naye akasema katika Luka 17:26-30 kwamba kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na Lutu ndivyo itakavyokuwa katika siku ambapo Mwana wa adamu angerudi duniani.

Hata baada ya Mfalme Farao kupigwa na baa moja baada ya nyingine yeye aliendelea kufanya moyo wake kuwa mgumu ndipo akapata maangamizi. Basi badala ya ulimwengu wa sasa kufanya moyo wake kuwa mgumu tunahitaji kutubu na kumwelekea Mungu ili tupate jawabu la kudumu, sio tu kutokana na virusi vya koronavirus (COVID-19) bali pia kutokana na adhabu ya dhambi.

Hebu basi tumwombe Mungu hadi hapo atakaponyoosha mkono wake wa rehema kutuelekeza sisi wanadamu. Hebu tujihukumu sisi wenyewe, tujue nyakati tunazoishi, na kuchunga nafsi zetu. Bwana wetu yuko langoni na atarudi hivi karibuni kuleta hukumu yake.

Omani, sio Woga

NYINYI NI CHUMVI YA ULMIMWENGU

NDUGU PAUL PHILLIPS (CALIFORNIA, MAREKANI)



“Nyinyi ni chumvi ya ulimwengu . . .” Je, wewe umeliwaza kwa kiwango kipi swala ambalo linazungumziwa ulimwenguni kote? Mawazo yako juu ya swala hili ni yapi? Mimi nimechunguza misimamo ya baadhi ya watu walio karibu nami kuhusiana na swala hili. Baadhi ya

mielekeo yao imetokana na woga? Mielekeo mingine imetokana na wao kuliwaza swala hili kwa makini. Je, wewe Mkristo mwenzangu, msimamo wako ni upi kuhusiana na swala hili? Je, umedumisha amani yako hata unapoliwaza swala hili ambalo limekumba jamii zetu? Je, unao utulivu ndani ya moyo wako? Je, umesimama wima bila wasiwasi wowote katika janga hili? Sisi tumeitwa ili tuwe baraka; maisha yetu yanatakiwa kuwa chanzo cha wokovu na udumishaji wa ulimwengu dhidi ya uzorotaji wake.

Nikifikiria kuhusu yale ambayo nimeona yafuatayo ndiyo mawazo yangu: huu sio wakati wetu kuogopa, bali ni wakati wetu kukua. Ni wakati wa mtu kutambua umuhimu wa wokovu wa kweli, wokovu ambao unampatia mtu amani ambayo haieleweki kwa kutumia akili za kibinadamu,

chanzo cha amani hiyo kikiwa ni upendo wa Mungu ambao humwondolea mwanadamu woga wa maangamizi. Sisi tumepokea ahadi za Mungu Mkuu! “Je, ni jambo gani ambalo Yeye anaweza kusema kuliko kile ambacho tayari ashasema . . .” Sikiliza maneno yake! Imani yako iko wapi? Tumaini lako liko wapi? Msingi wa maisha yako ni upi? Tukiwa kwenye dhoruba za maisha ndipo tunajua kile ambacho tuko nacho, na kile ambacho hatuna. Sisi tumebarikiwa kwa kupata msimamo kama huo ndani yake Mungu, msimamo ambao unatuonyesha kile ambacho tuko nacho ndani mwetu! Je, si ni kitu cha thamani kuu sisi kujua msimamo wetu kulingana na Neno la Mungu?

Kuna ahadi ambayo mimi nimeandika kwenye kijikaratasi changu na ambayo mimi hukitazama muda baada ya mwingine, ili inikumbushe na niwakumbushe wale wengine neno la kweli la Mungu wetu Mkuu: “Kwa kuwa BWANA, Mungu, ni jua na ngao, BWANA atatoa neema na utukufu. Hatawanyima kitu chema hao waendao kwa ukamilifu. Ee BWANA wa majeshi, heri mwanadamu anayekutumaini Wewe” (Zaburi 84:11-12).

KUWA MBALI NA WENZAKO AU KUPATANA KIROHO?



“Kuwa mbali wa wenzako” ni maneno ambayo yanatumika sana kwa sasa. Maana ya jambo hili ni mtu kuongeza nafasi iliyopo kati yake na mwenzake (tuseme futi sita hivi), ili kujikinga dhidi ya kusambaziwa virusi vya koronavirus (COVID-19). Mwongozo huu pia unawataka watu kujitenga na vikundi vya watu, na ni jambo ambalo limesababisha biashara na mashule kufungwa. Hii ni kumaanisha kwamba watu wengi wanakaa nyumbani mwao bila kutangamana na watu wale wengine, na bila kuhudhuria ushirika wa kila wiki wa Wakristo, na hata bila kupata msaada wa watu wale wengine.

Lakini huu ni wakati mwafaka wa sisi “kupatana kiroho.” Kwanza kabisa tumia wakati huu kupatana zaidi na Bwana

Yesu na uweke nguvu uhusiano wako na Mungu. Pili, hata ingawa hutaweza kupatana kimwili na mtu yule mwingine, unaweza kuendelea kuwa rafiki yake. Chukua muda kila siku kuwafikia watu wale wengine kwa kuwaandikia ujumbe mfupi, kuandika kwenye mitandao ya kijamii, na kuwapigia wenzako simu ili kuongeza mapatano ya kiroho ambayo yako kati yako na watu wale wengine, na ili uwaongoze kumwona Yesu katika matukio haya yaliyotupata. Kuna watu wengine ambao wanahisi kuwa upweke, wakijihisi kwamba wako peke yao, na kujaa woga. Serikali zetu zimesema watu wawembali na wenzao, lakini Bwana anasema tupatane kiroho. Wewe unaweza kuwa mwangaza kwa mwenzako hata katika siku hizi ngumu tunazoishi. —mws

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA




MAVAZI YALIYOPANGWA VIZURI



NDUGU ED WILSON (OKLAHOMA, MAREKANI)

Katika Yohana 20:6-8 hadithi ya kufufuka kwa Yesu inasema hivi, “Basi akaja na Simoni Petro, akaingia ndani ya kaburi; akavitazama vitambaa vilivyolala, na ile lesu iliyokuwako kichwani pake; haikulala pamoja na vitambaa, bali imezongwa-zongwa mbali mahali pa peke yake. Basi ndipo alipoingia naye yule mwanafunzi mwingine (Yohana) . . . akaona na kuamini.”

Mtume Yohana alifika katika kaburi lililokuwa tupu na kupata nguo ambazo Yesu alizikwa nazo kama zimepangwa vizuri, huku kitambaa ambacho kilikuwa chini ya kichwa chake kikiwa kimetengwa na nguo zile zingine. Ndipo Yohana akapata ufunuo wa ajabu na kuweza kutambua kwa ghafla ujumbe ambao Yesu alikuwa amewaachia: mwili wake haukuwa umeondolewa kwa ghafla. Hii haikuwa kazi ya adui ambaye alikuwa akijaribu kunyang’anya wanafunzi hawa hata faraja ndogo ya kumkaribia hayati mpendwa wao. Pia ni kusema kwamba hii haikuwa kazi ya marafiki wa Yesu kwa maana hawangekosea mwili wa mpendwa wao Yesu heshima kwa kiwango hiki hata kufikia kuchukua mwili huo ukiwa uchi. Hapana. Ilikuwa dhahiri kwamba mtu huyu ambaye juzi tu walimwona akiishi siku zake za mwisho za uhai wake wa kibinadamu alikuwa amejifanyia tendo hili ambalo alikuwa amesababisha kufanyika kwa rafiki yake Lazaro, wakati Yeye aliagiza kwamba Lazaro afunguliwe kutoka kwa mavazi aliyokuwa amezikwa nayo na ambayo yalikuwa yamemfunga.



Pia ilionekana kwamba Yeye hakutoka kaburini akiwa kama mtu ambaye hajifahamu, ambaye akili zake sasa zimeanza kumrudia, na ambaye ametambua janga lililokuwa limempata na kumfanya kutoroka. Kwa utulivu mkubwa na uamuzi wa kibinafsi, na katika utukufu wa Utawala wake juu ya kifo, na bila kuwa na haja ya kusumbuka kwa ajili ya uwepo wa askari na Mafarisayo, Yeye aliamka kutoka mahali pale alikuwa amelalishwa na kufanya kuwe na mpango mahali ambapo watu wengine walikuwa wamechanganyikiwa sana. Muhstasari wa swala hili la mavazi ambalo sasa Yohana alishaelewa vizuri umetolewa kwa maneno yanayosema kwamba “. . . akaamini.” Hii ilikuwa hatua muhimu sana katika kukua kwa imani ya ya Yohana na yeye akaongozwa na Roho wa Mungu kuandika maneno hayo ili wewe na mimi tuweze kufaidika.